

## **NJAA KATIKA NCHI**

Katika makala hii, tunataka kutafakari maneno yaliyopo katika Amosi 8:11-14, kuhusiana na somo la “njaa katika nchi.” Kwa kufanya hivyo, tunataka kulichunguza fungu lote la maandiko na kulihusha na taifa la Israel ambao ndiyo walioandikiwa na kisha kwetu leo. Wakati wa mahubiri ya Amosi, Taifa la Israeli likikuwa katika wakati wa ustawi kiuchumi. Kwa upande mwininge, likikuwa na uonevu mwiningi, ulafi, starehe na anasa. Hali yao kidini ilikuwa sawa na hali yetu leo kwa kiasi kikubwa. Kulikuwa na ibada nyingi, bali haki ilikuwa kidogo. Kule Dani, Beersheba, Gilgali na Betheli likikuwa kunafanyika ibaada za sanamu. Kulikuwa na uozo mkubwa wa kimaadili katika Israeli.

Kutokana na kudharau mafundisho ya nabii Amosi, Bwana akawaeleza Israeli juu ya njaa ambayo ilikuwa inawajilia. Isingejuwa ni njaa inayotokana na upungufu wa chakula na kinywaji. Ingawaje pia hakusema kuwa kusingekuwako njaa ya jinsi hiyo. Lakini, njaa aliyoizungumzia ingehusu mambo ya kiroho. Siku zote, mwanadamu humgeukia Bwana wakati wa shida kubwa na taabu. Na sasa Bwana alikuwa anasema kusingewako ujumbe kutoka kwake tena kuititia manabii. Israeli walikuwa wamewafukuza na kuwadhalilisha manabii waliokuwa wanatangaza neno la Bwana. Sasa, Waisraeli watakapokuwa wanamgeukia Mungu na kutafuta mwongozo kutoka kwa manabii, hakuna nabii ambaye angewajilia.

Ilikuwa ni balaa kiasi gani! Fikiria ingekuwaje kama unamgeukia Bwana ili akujibu halafu unakuta hayupo. Kwa sababu ya ubinaksi wao, Israeli walimfanya Bwana ageukie mbali nao. Katika mstari wa 12 maelezo yanatolewa ya kuvutia kuhusiana na Israeli “...nao watatanga toka bahari hata bahari...” Neno “kutangatanga” limetumika ili kuelezea hali ya utafutaji isiyo thabitia anayokuwa nayo mtu aliyechanganyikiwa. Huwakilisha wale wanaotafuta kitu wasichojuu mahali pa kukipata. Hivyo, Israeli wameelezewa kuwa kama watu waliochanganyikiwa na kuhanyahanya, warandaranda kutoka bahari hadi bahari, wakienda na kurudi, wakitafuta neno la Bwana bila kuweza kuliona.

Wazo lilo hilo linaonekana katika Waefeso 4:14. Inaweza kuwa vigumu kwetu sisi kuelewana na hili pengine kwa sababu neno la Bwana lipo. Tunaweza kupata taswira tofauti tukilitazama hili kwa mtazamo wa kimwili.

Tukilitazama kwa mtazamo wa chakula na maji, tutang’amua kwa urahisi. Leo tukiangalia fungu letu hili la maandiko na kutazama huku na huko tunaona njaa katika nchi. Siyo iliyoletwaa na Mungu, au msimu, la, ni njaa tulijojitakia wenyewe. Linapokuja suala la kiroho tunadhikika wazi wazi ingawaje hatujafikia kiwango cha kushindwa kuliona neno la Bwana. Hasa unapotokea upungufu wa maarifa ya neno la Mungu leo ambao haujapata kutokea. Tunawasikia watu wakisema tena na tena “siwezi kuilewa Biblia” wakati tukiangalia huko nyuma wazazi, babu na bibi zao, Biblia haikuwapa taabu. Nao hawakuwa wasomi katika Nyanja nyingi ukilinganisha na wale wanaodai kuwa wanashindwa kuilewa Biblia.

Nionalo, si suala la “nashindwa” bali ni “sitaelewa” linapokuja suala la kuyaelewa mapenzi ya Bwana. Tumejitakia wenyewe njaa katika nchi Linapokuja suala la kuelewa neno la Bwana tunakuwa tumevimbiwa ulimwengu, na hii ni hiari yetu wenyewe. Tumeacha;

“Kulificha neno la Mungu miyoni mwetu” (Zaburi 119:11)  
“Kuchunguza maandiko” (Yohana 5:39)  
“kuchunguza maandiko ili kuona kama mambo haya ndivyo yalivyo”  
(Matendo 17:11)  
“Kujitahidi kujionyesha kuwa tumekubaliwa na Mungu” (2 Timotheo 2:15)

Na kwa sababu hii, kibiblia tumevimbwa. Namna pekee ya kutuwezesha kurekebisha tatizo hili ni kurudi kuwa watu wa kitabu. Zamani watu wa Mungu walijulikana kwa kiwango chao cha ufahamu wa Biblia. Nasikitika kusema kuwa jambo hili halipo tena!

Sababu ya hili ni kwamba tunatumia muda mwingi kwenye magazeti, luninga, Facebook, au mamia ya mambo mengine kuliko tunavyokuwa na Biblia. Na kwa kadri tunavyoendelea na haya, daima kutakuwa na “njaa katika nchi”. Njaa ambayo siyo tu itatuathiri sisi milele na milele, bali na watoto wetu, wajukuu zetu na nyanya zetu pia endapo ulimwengu huu utadumu kwa kiasi hicho.

Kwa mara nyingine, tunatakiwa kuwa watu wa Kitabu. Kama baba zetu wa kiroho walivyokuwa nasi tunatakiwa kuwa wanafunzi wa Neno. Hili litakapotendeka, njaa itaondoka katika nchi, lakini hadi litendeke njaa itaendelea kuongezeka.